MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2017/18

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO
NOVEMBA, 2016

ISBN 978 - 9987 - 829 - 02 - 9

YALIYOMO

1.0 **UTANGULIZI** 1

2.0 **MABORESHO YA MFUMO WA KIBAJETI** 2
2.1 Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015 2
2.2 Uandaaji wa Bajeti kwa Kuzingatia Programu 2
2.3 Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Miradi ya Umma wa Mwaka 2015 3

3.0 **UANDAAJI WA MIPANGO NA BAJETI** 3
3.1 Kamati za Bajeti 3
3.2 Ratiba ya Maandalizi ya Mipango na Bajeti 3
3.3 Kuhamishia Shughuli za Makao Makuu ya Serikali Dodoma 4
3.4 Mchakato wa Majadiliano na Uchambuzi wa Bajeti 4
3.5 Uingizaji wa Takwimu za Bajeti Katika Mfumo wa *IFMS* 6

4.0 **MAELEKEZO YA UANDAAJI WA MIPANGO NA BAJETI** 6
4.1 Mfumo wa Mapato na Matumizi Katika Kipindi cha Muda wa Kati 6
4.2 Viwango vya Ukomo wa Bajeti Katika Kipindi cha Muda wa Kati 7
4.3 Mikakati ya Kuongeza Mapato 7
4.4 Vigezo vya Kugawa Rasilimali Fedha 9
4.4.1 Matumizi ya Kawaida 9
4.4.2 Bajeti ya Maendeleo 11

5.0 **MAMBO MENGINE YA KUZINGATIWA KATIKA UANDAAJI WA MIPANGO NA BAJETI** 12
5.1 Kudhibiti Ulimbikizaji wa Madeni 12
5.2 Madeni Sanjari (Contingent Liabilities) 13
5.3 Hatua za Kudhibiti Matumizi na Kupunguza Gharama 13
5.4 Kiwango cha Kubadilisha Fedha 15
5.5 Kujumuisha Masuala Mtambuka Katika Mipango na Bajeti 15
5.6 Utawala Bora 15
5.7 Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi 16
5.8 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa 16
5.9 Usimamizi wa Mali za Umma 17
5.10 Ushirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Binafsi 18
5.11 Usimamizi wa Vihatarishi 19

6.0 **MAELEKEZO MAHSUSI KWA SEKRETARIETI ZA MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA** 20

7.0 **UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI TAARIFA YA UTEKELEZAJI** 22
7.1 Utoaji wa Taarifa za Utekelezaji 23
8.0 **HITIMISHO** 23

MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2017/18

1.0 UTANGULIZI

1. Mwongozo wa Mpango na Bajeti ni nyenzo ya kuandaa na kutekeleza bajeti ya Serikali na taasisi zake pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2017/18. Mwongozo wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2017/18 unaelekeza ukusanyaji wa mapato na utengaji rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Mpango huu ni wa pili katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21). Mwongozo umeandaliwa kwa mujibu wa Kifungu Na. 21 cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015 pamoja na kanuni zake.

2. Mwongozo wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2017/18 umezingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya Mwaka 2015; Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akizindua Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 20 Novemba, 2015; Maamuzi ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuhamishia shughuli za Makao Makuu ya Serikali Dodoma; Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano; na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) sanjari na makubaliano ya kikanda, makubaliano baina ya Tanzania na nchi nyingine na makubaliano ya kimataifa yaliyoridhiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

3. Lengo kuu la Mwongozo wa Mpango na Bajeti ni kuwaelekeza Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Umma namna ya kuandaa na kutekeleza mipango na bajeti kwa mwaka 2017/18.

4. Mwongozo wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2017/18 umegawanyika katika maeneo nane (8) ambayo ni: Utangulizi; Maboresho ya Mfumo wa Kibajeti; Uandaaji wa Mipango na Bajeti; Maelekezo ya Uandaaji wa Mipango na Bajeti; Mambo Mengine ya Kuzingatia katika Maandalizi ya Mipango na Bajeti; Maelekezo Mahsusi kwa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji Taarifa; na Hitimisho. Aidha, Mwongozo huu unapaswa kusomwa pamoja na kiambatisho chake.

2.0 MABORESHO YA MFUMO WA KIBAJETI

5. Serikali imefanya maboresho mbalimbali katika mfumo wa kibajeti ili kuongeza ufanisi, uwajibikaji na uwazi. Maboresho makubwa yaliyofanyika ni pamoja na kuandaliwa na kupitishwa kwa Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 na Kanuni za Bajeti za mwaka 2015; kuandaa Mfumo wa Programu wa Kibajeti; utekelezaji wa Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma Awamu ya Nne; pamoja na kupitishwa kwa Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Miradi ya Umma wa mwaka 2015.

2.1 Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015

6. Lengo kuu la Sheria ya Bajeti ni kuhakikisha kuwa usimamizi na uwajibikaji katika hatua zote za mchakato wa bajeti unazingatiwa. Hivyo basi, Maafisa Masuuli wote wanatakiwa kuendelea kuzingatia Sheria ya Bajeti pamoja na Kanuni zake wakati wa uandaaji na utekelezaji wa Mipango na Bajeti zao.

2.2 Uandaaji wa Bajeti kwa Kuzingatia Programu

7. Serikali imedhamiria kuandaa bajeti kwa kuzingatia Mfumo wa Programu (Programme Based Budget-PBB) ili kuwezesha utekelezaji wa bajeti kwa kuzingatia vipaumbele na kuongeza ufanisi katika kutoa huduma kwa umma. Mabadiliko haya yanatokana na maboresho mbalimbali yanayofanyika katika taasisi za kimataifa zinazosimamia masuala ya bajeti na fedha za umma. Mfumo huu utaanza kwa hatua ya majaribio katika Wizara nane (8) ambazo zimepatiwa mafunzo ya utekelezaji. Wizara hizo ni: Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; Wizara ya Maji na Umwagiliaji; Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi; Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Wizara ya Fedha na Mipango; Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji; pamoja na Wizara ya Nishati na Madini.

8. Mfumo huu unawataka Maafisa Masuuli wa Wizara za majaribio kuainisha bajeti zao kwa utaratibu wa programu na kwa kuzingatia miongozo na viwango vya kimataifa. Aidha, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuandaa bajeti kivuli za mafungu yao kwa kuzingatia

malengo ambayo yataonesha matokeo na viashiria vya kiutendaji vitakavyotumika kupima matokeo ya utekelezaji wa programu husika.

2.3 Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Miradi ya Umma wa Mwaka 2015

9. Mwaka 2015 Serikali ilitoa Mwongozo wa Uandaaji na Usimamizi wa Miradi ya Uwekezaji wa Umma ambapo mafunzo ya Mwongozo huo kwa watendaji wa mafungu mbalimbali yamefanyika mwaka 2016. Mwongozo huo, unatoa maelekezo mbalimbali ikiwemo: uibuaji na uchambuzi; ugharamiaji; utekelezaji; usimamizi; ufuatiliaji na tathmini; pamoja na usimamizi wa kanzi data ya miradi ya uwekezaji wa umma. Hivyo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia Mwongozo huo na kuhakikisha wanajenga uwezo wa wataalam kulingana na mahitaji ya mafungu yao.

3.0 UANDAAJI WA MIPANGO NA BAJETI

3.1 Kamati za Bajeti

10. Kifungu cha 18(2) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 kinaelekeza kuundwa kwa Kamati za Bajeti katika Serikali na taasisi zake ili kurahisisha maandalizi ya mipango na bajeti. Kamati za Bajeti zinaelekezwa kutekeleza majukumu yao katika uandaaji wa mipango na bajeti kama ilivyoainishwa katika Kanuni ya 17(3) ya Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015. Aidha, Maafisa Masuuli wa Taasisi na Wakala wa Serikali wanaelekezwa kuzingatia Nyaraka za Msajili wa Hazina katika uandaaji wa mipango na bajeti zao.

3.2 Ratiba ya Maandalizi ya Mipango na Bajeti

11. Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi na Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaelekezwa kuandaa kitabu cha Muundo wa Bajeti ya Muda wa Kati - *MTEF* na kukiwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango wiki ya kwanza ya Februari, 2017 kwa ajili ya uchambuzi. Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaagizwa kuandaa na kuwasilisha makadirio yao Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI) wiki ya tatu ya Januari, 2017 baada ya kupitishwa na mamlaka husika kwa ajili ya uchambuzi.

12. Wizara ya Fedha na Mipango itafanya majumuisho ya bajeti za Mafungu na kuwasilisha kwenye ngazi za maamuzi za Serikali. Aidha, Mafungu yataandaa Randama za bajeti zao na kuwasilisha kwenye Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta wiki ya tatu ya Machi, 2017 na wiki ya kwanza ya Aprili, 2017 kwa ajili ya uchambuzi na kuandaa mapendekezo yatakayowasilishwa Bungeni. Majumuisho ya bajeti yatawasilishwa Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa kuanzia wiki ya pili ya Aprili, 2017 hadi wiki ya nne ya Juni, 2017. Utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2017/18 utaanza tarehe 1 Julai, 2017 hadi tarehe 30 Juni, 2018.

3.3 Kuhamishia Shughuli za Makao Makuu ya Serikali Dodoma

13. Ratiba ya maandalizi ya kuhamisha shughuli za Makao Makuu ya Serikali Dodoma itatekelezwa kwa awamu katika muda wa kati. Katika mwaka 2017/18, Maafisa Masuuli wanatakiwa wajumuishe mahitaji ya kuhamia Dodoma katika mipango na bajeti kwa kuzingatia ratiba iliyotolewa na Serikali. Mipango ya ujenzi wa majengo na miundombinu ya Serikali iliyopangwa kujengwa Dar es salaam ihamishiwe Dodoma. Aidha, ujenzi wa majengo na miundombinu yoyote inayotegemewa kujengwa Dodoma ni lazima upate idhini kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu.

3.4 Mchakato wa Majadiliano na Uchambuzi wa Bajeti

14. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuandaa na kuwasilisha rasimu ya mipango na bajeti katika Mabaraza ya Wafanyakazi kama ilivyoelekezwa katika Sheria ya Majadiliano ya Pamoja Katika Utumishi wa Umma SURA 105.

15. Uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Umma utafanywa kwa pamoja baina ya Wizara ya Fedha na Mipango; Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Ofisi ya Msajili wa Hazina na wadau wengine. Taasisi zote za Serikali zinaagizwa kuandaa na kuwasilisha mipango na bajeti zao Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya uchambuzi kwa

mujibu wa Kifungu cha 22(1) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015.

16. Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi na Wakala wa Serikali, Sekretariati za Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinapaswa kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango nakala tano (5) ngumu na laini za rasimu ya mipango na bajeti zao kwa ajili ya uchambuzi wa kitaalamu. Vile vile, zinapaswa kuwasilisha nakala tatu (3) za mipango na bajeti iliyosainiwa kwa mamlaka tajwa. Mikoa na Halmashauri zinapaswa kuwasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI nakala tatu (3) za MTEF zilizosainiwa. Pia, Taasisi za Umma zinatakiwa kuandaa mipango na bajeti na kuwasilisha nakala tatu (3) zilizosainiwa kwa Wizara zinazoratibu bajeti zao na Ofisi ya Msajili wa Hazina. Ili kuweka ufafanuzi na uwazi katika zoezi la uchambuzi wa bajeti, majadiliano yataendeshwa kwa kuzingatia yafuatayo:

    i. Kupitia utekelezaji wa bajeti ya mwaka uliopita (2015/16);
    ii. Kupitia mapato na matumizi ya kipindi cha nusu mwaka wa 2016/17, changamoto na hatua zilizochukuliwa kukabiliana nazo;
    iii. Kitabu cha Muundo wa Bajeti ya Muda wa Kati - *MTEF* kama ilivyoelekezwa katika Sura ya Tano ya Kiambatisho cha Mwongozo;
    iv. Vipaumbele vilivyotolewa katika Mwongozo na ukomo wa bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango;
    v. Kuwasilisha mipango na bajeti iliyoandaliwa kwa Mfumo wa Utengaji Bajeti wa Kimkakati (*Strategic Budget Allocation System – SBAS*) kwa upande wa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali na Sekretarieti za Mikoa, na pia *PlanRep* kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa;
    vi. Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Miradi ya Umma wa mwaka 2015; na
    vii. Maelekezo ya Mwongozo wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2017/18, Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 na Kanuni zake za mwaka 2015, Nyaraka za Msajili wa Hazina, pamoja na Nyaraka na Miongozo mingine ya Serikali.

3.5 Uingizaji wa Takwimu za Bajeti Katika Mfumo wa *IFMS*

17. Kulingana na ratiba ya maandalizi na uchambuzi wa bajeti, Maafisa Masuuli wote wanatakiwa kutekeleza yafuatayo:
    i. Kukamilisha kwa wakati zoezi la kuingiza takwimu za bajeti kwenye mfumo wa *IFMS* na kuhakikisha usahihi wa takwimu hizo;
    ii. Kuzingatia Mfumo wa Kimataifa wa mwaka 2014 wa Takwimu za Kifedha za Serikali (*GFS Codes*) toleo la mwaka 2014 na za miradi (*Project Codes*) kama ilivyotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango;
    iii. Kutumia vizio vilivyokubalika na vinavyotolewa katika mfumo wa *SBAS* na *PlanRep*; na
    iv. Kuweka makadirio sahihi ya gharama za kodi ya pango, umeme, maji na simu.

4.0 MAELEKEZO YA UANDAAJI WA MIPANGO NA BAJETI

4.1 Mfumo wa Mapato na Matumizi Katika Kipindi cha Muda wa Kati

18. Kwa kuzingatia malengo ya Sera za Uchumi jumla na Bajeti kwa mwaka 2017/18, Sura ya Bajeti inaonesha kuwa jumla ya Shilingi bilioni 32,945.8 zinatarajiwa kukusanywa na kutumika katika kipindi hicho. Kiasi hiki ni makisio ya awali ambapo makisio ya mwisho yatapatikana baada ya kukamilika kwa tathmini ya nusu mwaka pamoja na taarifa ya Kikosi Kazi cha Maboresho ya Kodi kinachojumuisha wadau mbalimbali pamoja na makubaliano na Washirika wa Maendeleo. Makisio haya yanajumuisha mapato ya kodi Shilingi bilioni 18,097, mapato yasiyo ya kodi Shilingi bilioni 2,022 na mapato ya Halmashauri Shilingi bilioni 753.3. Serikali inatarajia kupata kiasi cha Shilingi bilioni 3,699.8 ikiwa ni misaada na mikopo nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo na mikopo ya ndani inatarajiwa kuwa Shilingi bilioni 6,293.5. Vile vile, Serikali inatarajia kukopa kiasi cha Shilingi bilioni 2,080.2 kama mikopo ya nje yenye masharti ya kibiashara.

19. Katika mwaka 2017/18, Serikali inapanga kutumia jumla ya Shilingi bilioni 32,945.8 kulingana na maeneo ya vipaumbele yaliyoainishwa katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21) na Mwongozo huu. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 19,782.3 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ikijumuisha Shilingi bilioni 7,205.8 kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Serikali, Shilingi bilioni 2,853.1 kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shilingi bilioni 9,723.4 kwa ajili ya Deni la Taifa. Aidha, matumizi ya maendeleo yatakuwa Shilingi bilioni 13,163.5 ambapo kiasi cha Shilingi bilioni 9,960 ni fedha za ndani na Shilingi bilioni 3,203.5 ni fedha za nje.

4.2 Viwango vya Ukomo wa Bajeti Katika Kipindi cha Muda wa Kati

20. Viwango vya ukomo wa bajeti kwa ajili ya maandalizi ya bajeti ya Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa vitatolewa kwa kuzingatia vigezo vya ugawaji rasilimali na vipaumbele vilivyoainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Mwongozo huu. Aidha, hakutakuwa na nyongeza ya ukomo wa bajeti nje ya viwango vitakavyotolewa. Kwa msingi huo, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuzingatia ukomo wa viwango vya bajeti vitakavyoidhinishwa kwa mwaka 2017/18.

4.3 Mikakati ya Kuongeza Mapato

21. Serikali imeandaa mikakati na hatua za kuongeza na kuimarisha ukusanyaji wa mapato kama ilivyoainishwa katika Sura ya Nne ya Kiambatisho cha Mwongozo huu. Jukumu la kusimamia ukusanyaji wa mapato yote ya Serikali ni la Wizara ya Fedha na Mipango. Aidha, Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa zitakusanya mapato kwa niaba ya Wizara ya Fedha na Mipango na kuwasilisha kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Mapato hayo yatagawiwa kulingana na bajeti zitakazoidhinishwa katika mafungu yao. Aidha, Taasisi na Wakala za Serikali zinaelekezwa kuendelea na akaunti zao za mapato zilizopo Benki Kuu na kuwa na akaunti ya ukusanyaji wa mapato na matumizi katika benki za biashara. Ili kutimiza lengo hili, Taasisi na

Wakala zote zinatakiwa kuwasilisha mapato yote katika akaunti ya Benki Kuu ndani ya saa 24 baada ya kukusanywa.

22. Mgao wa fedha kutoka akaunti za mapato zilizo Benki Kuu kwenda kwenye akaunti za matumizi za Taasisi zilizo katika benki za biashara utazingatia Mpango wa Mtiririko wa Fedha wa bajeti iliyoidhinishwa. Fedha kwa ajili ya matumizi ya Taasisi na Wakala za Serikali zitasimamiwa na Msajili wa Hazina kulingana na Mpango Kazi na Mtiririko wa Fedha na bajeti iliyoidhinishwa.

23. Maafisa Masuuli wote wanaelekezwa kuweka mazingira wezeshi katika kufanikisha ukusanyaji wa mapato kwa kufanya yafuatayo:
    i. Kuainisha vyanzo vyote vya mapato kama moja ya mkakati wa kuboresha ukusanyaji wa mapato;
    ii. Kuhakikisha kuwa majengo yote yanathaminishwa kulingana na bei halisi ya soko. Aidha, majengo ambayo hayajafanyiwa uthamini yatozwe kodi kwa viwango vinavyofanana kwa majengo ya kila kundi. Zoezi hili lifanyike kwa kipindi cha mpito wakati zoezi la uthamini wa majengo hayo likikamilishwa;
    iii. Kupima na kuainisha matumizi ya ardhi kwa ajili ya utoaji wa hati miliki ya ardhi;
    iv. Urasimishaji wa biashara na mali ili kupanua wigo wa kodi;
    v. Kupitia upya ada, ushuru na tozo ili kuzirekebisha ziendane na maendeleo ya kiuchumi na kijamii;
    vi. Kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa kodi, ada, ushuru na tozo ili kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato;
    vii. Kuingia mikataba na wazabuni, makandarasi na watoa huduma wanaotumia mashine za *EFD*;
    viii. Kutoingia mikataba inayohusisha misamaha ya kodi bila idhini ya Waziri wa Fedha na Mipango; na
    ix. Kuimarisha ukaguzi na usimamizi wa vituo vya ukusanyaji wa mapato kama vile bandari, viwanja vya ndege, na mipakani.

24. Maafisa Masuuli wote wanatakiwa kuhakikisha kuwa makadirio na makusanyo ya mapato yote yanajazwa kwenye fomu Na. 4 ili kuhakikisha vyanzo vyote vya mapato vinaainishwa, takwimu za makusanyo ya mapato zinakuwa sahihi na maoteo ya mapato yanawiana na fursa zilizopo katika kila chanzo.

4.4 Vigezo vya Kugawa Rasilimali Fedha

25. Makadirio ya matumizi ya Serikali yamegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo.

4.4.1 Matumizi ya Kawaida

a) Mishahara

26. Bajeti ya mishahara kwa watumishi wa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa zizingatie maeneo makuu matano ambayo ni: watumishi waliopo, upandishwaji vyeo, nyongeza ya mishahara ya kila mwaka, ajira mpya, na michango ya kisheria. Katika maandalizi ya bajeti ya mishahara, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuzingatia maelekezo na nyaraka zilizotolewa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Taasisi za Umma zizingatie maelekezo yaliyotolewa na Ofisi ya Msajili wa Hazina. Hivyo, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuzingatia yafuatayo:

(i) Kutumia taarifa za rasilimali watu zilizohakikiwa na ikama katika kuandaa bajeti ya mshahara iliyopitishwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora;

(ii) Kutumia Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Rasilimali Watu;

(iii) Kutambua mahitaji ya ikama kwa kufanya tathmini ya watumishi waliopo kwa kulinganisha na kibali kilichotolewa ili kuwasilisha taarifa ya ikama Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kupitia Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Rasilimali Watu;

(iv) Bajeti kwa ajili ya posho za kukaimu nafasi za uongozi zinazosubiri uteuzi zitengwe katika bajeti ya mishahara. Aidha, posho za kukaimu nafasi za uongozi zinazotokana na ugonjwa, likizo na safari zitaendelea kukasimiwa katika bajeti ya matumizi mengineyo; na

(v) Michango ya kisheria na ya kiinua mgongo kwa watumishi wenye ajira za mikataba ikadiriwe kwa usahihi.

27. Katika mwaka 2017/18, kipaumbele cha ajira mpya kitatolewa katika sekta zenye upungufu wa watumishi. Sekta hizo ni: Elimu (walimu wa Sayansi, Hisabati na Fundi Sanifu wa Maabara); Afya (Madaktari,

Wauguzi na Watalaam wa Chakula na Lishe); Kilimo na Mifugo (Maafisa Ugani) na Nishati (mafuta na gesi). Aidha, katika sekta nyingine ajira mpya zitategemea uwepo wa rasilimali fedha na nafasi za kazi.

b) Huduma za Mfuko Mkuu wa Hazina

28. Katika kusimamia matumizi ya Mfuko Mkuu wa Hazina, Serikali itafanya uchambuzi wa makadirio ya ulipaji wa Deni la Taifa, michango ya mwajiri katika mifuko ya hifadhi za jamii, na michango ya mwajiri kwa watumishi walio kwenye mikataba. Aidha, kasma ya bajeti hizi itatengwa katika Fungu 22 – Deni la Taifa na kusimamiwa na Wizara ya Fedha na Mipango.

c) Matumizi Mengineyo

29. Maafisa Masuuli wote wanaelekezwa kuhakikisha wanatenga fedha kwa ajili ya matumizi yasiyoepukika pamoja na majukumu ya msingi katika mafungu yao. Aidha, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutenga fedha ili kulipa madai ya watoa huduma na wazabuni kwa lengo la kuepuka malimbikizo ya madeni na kupunguza gharama za riba.

d) Upelekaji wa Fedha za Ruzuku kwa Serikali za Mitaa

30. Serikali itaendelea kutoa ruzuku kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuboresha utoaji wa huduma katika maeneo yao. Ruzuku hizo zitatolewa kwa mfumo wa ruzuku jumuishi, ruzuku ya maendeleo ya Serikali za Mitaa pamoja na mifumo mingine ya fedha za maendeleo. Ukomo wa bajeti unakadiriwa kwa kutumia matokeo ya upimaji wa utendaji kazi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na vigezo vya ugawaji wa rasilimali. Katika uandaaji wa mipango na bajeti, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaelekezwa kuzingatia mambo yafuatayo:

(i) Ruzuku ya uendeshaji *(capitation)* kwa Shule za Msingi itaendelea kuwa shilingi 10,000 kwa kila mwanafunzi kwa mwaka ikijumuisha wanafunzi wa shule za awali na maalum. Aidha, asilimia 40 ya fedha zitaendelea kutumika kwa ajili ya ununuzi wa vitabu katika utaratibu wa ununuzi wa pamoja na kiasi kinachobaki cha asilimia 60 kitatumwa moja kwa moja kwenye akaunti za shule;

(ii) Ruzuku ya uendeshaji *(capitation)* kwa Shule za Sekondari itaendelea kuwa shilingi 25,000 kwa kila mwanafunzi wa kutwa na bweni kwa mwaka. Asilimia 50 ya fedha zitaendelea

kutumika kwa ajili ya ununuzi wa vitabu katika utaratibu wa ununuzi wa pamoja na kiasi kinachobaki cha asilimia 50 kitatumwa moja kwa moja kwenye akaunti za shule;

(iii) Kigezo cha kutenga fedha kwa ajili ya chakula cha wanafunzi kitaendelea kuwa shilingi 540,000 (Shilingi 2,000 x Siku 270 za shule) kwa mwaka kwa kila mwanafunzi aliyesajiliwa kwenye Shule za Msingi na Sekondari za Bweni; na

(iv) Uandaaji wa bajeti za mitihani ya Shule za Msingi na Sekondari uzingatie viwango halisi vya mahitaji.

4.4.2 Bajeti ya Maendeleo

31. Katika kuandaa mipango na bajeti ya mwaka 2017/18, Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Umma zinatakiwa kuzingatia maeneo ya vipaumbele kama yalivyoainishwa kwenye Sura ya Tatu ya Kiambatisho cha Mwongozo huu na kutumia Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Miradi ya Umma wa Mwaka 2015. Hivyo, Maafisa Masuuli wanatakiwa kutoa kipaumbele katika maeneo yafuatayo:

(i) Miradi ya miundombinu inayoendelea ili ikamilishwe kabla ya kuanza kutekeleza miradi mipya;

(ii) Kulipa madeni ya makandarasi kwa wakati;

(iii) Ugawaji wa rasilimali utoe kipaumbele kwenye miradi ya kielelezo kwa ajili maendeleo ya viwanda kama iliyoanishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano;

(iv) Kufanya uthamini wa ardhi na majengo kwa ajili fidia ya maeneo ya kimkakati ya uwekezaji wa viwanda;

(v) Kufanya utafiti wa viwanda vinavyotumia malighafi zinazozalishwa ndani ya nchi ili kuchochea ukuaji wa uchumi;

(vi) Kuanzisha kongani za viwanda na kuwezesha upatikanaji wa teknolojia rahisi na nafuu ya viwanda; na

(vii) Miradi ya kimkakati iliyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2017/18 na kuandaliwa kwa kuzingatia Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Miradi ya Umma wa mwaka 2015.

32. Miradi inayotekelezwa kwa zaidi ya mwaka mmoja ni lazima ihakikiwe na Wizara ya Fedha na Mipango kwa mujibu wa Kifungu

Na. 51 cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 na Sheria ya Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Binafsi *(PPP)* Na. 18 ya mwaka 2010 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2014. Aidha, ruzuku ya Maendeleo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa itatolewa kwa kuzingatia mapitio ya vigezo vilivyopo kwenye Mwongozo wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

33. Kwa upande wa fedha za nje za maendeleo, Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Umma zinatakiwa kuandaa bajeti kwa kuzingatia ahadi zilizothibitishwa na Washirika wa Maendeleo pamoja na kuhakikisha kuwa:
    (i) Mchango wa Serikali kwenye miradi ya ubia *(counterpart fund)* unatengewa bajeti;
    (ii) Miradi yote inayopata fedha za Washirika wa Maendeleo inajumuishwa katika bajeti ya Serikali;
    (iii) Miradi yote inayopata fedha za Washirika wa Maendeleo iwe na mikataba na kuwasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango; na
    (iv) Taarifa ya mapokezi ya fedha, vifaa na utaalam kwa miradi yote inayopata ufadhili wa moja kwa moja kutoka kwa Washirika wa Maendeleo *(D-Fund)* itolewe ndani ya kipindi cha robo mwaka husika.

5.0 MAMBO MENGINE YA KUZINGATIWA KATIKA UANDAAJI WA MIPANGO NA BAJETI

5.1 Kudhibiti Ulimbikizaji wa Madeni

34. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuwa utaratibu wa kupata mikopo kwa miradi mipya na inayoendelea uzingatie Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada SURA 134 kama ilivyorekebishwa mwaka 2004. Kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa, mapitio ya mkopo yatazingatia Sheria ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, SURA 290. Aidha, Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kupata idhini ya Waziri wa Fedha na Mipango kabla ya kukopa kama ilivyobainishwa katika Kifungu Na. 60(4) na 62(b) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015.

35. Maafisa Masuuli wanapaswa kuzingatia kifungu cha 52(1) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 pamoja na Waraka Na. 4 wa Mwaka 2014 wa Mlipaji Mkuu wa Serikali ili kuepuka ulimbikizaji wa madeni. Kutokana na hali hiyo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuchukua hatua zifuatazo:

(i) Kuweka kipaumbele katika utengaji wa fedha za kulipia madeni yaliyohakikiwa;
(ii) Kuhakikisha kwamba hakuna madeni mapya yanayozalishwa;
(iii) Kuingiza matumizi yote kwenye Mfumo wa Malipo wa IFMS;
(iv) Kubainisha madeni yaliyopo na kuhakikisha yanaingizwa kwenye hesabu za majumuisho za Serikali; na
(v) Kuhakikisha madeni yote yamehakikiwa na Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali na kuingizwa kwenye hesabu za fungu husika.

5.2 Madeni Sanjari (Contingent Liabilities)

36. Katika kusimamia na kudhibiti madeni sanjari *(contingent liability)* hususan yenye dhamana ya Serikali, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kufanya ufuatiliaji wa karibu wa mikataba inayoweza kusababisha madeni. Aidha, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia madeni sanjari yote katika maandalizi ya bajeti zao.

5.3 Hatua za Kudhibiti Matumizi na Kupunguza Gharama

37. Maafisa Masuuli wanapaswa kuendelea kutekeleza hatua za kubana matumizi katika maeneo wanayosimamia bila kuathiri huduma zinazotolewa. Hivyo, wanaelekezwa ifuatavyo:

i. Kuhakikisha Mikataba inayoingiwa na Serikali na taasisi zake inakuwa katika Shilingi za Kitanzania isipokuwa kwa mikataba inayohusisha biashara za kimataifa;
ii. Kuendelea kupunguza gharama na matumizi yasiyokuwa ya lazima ikiwemo sherehe za kitaifa, posho za vikao, uchapishaji wa fulana, kofia, mikoba, safari za nje, mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi na ununuzi wa samani kutoka nje;
iii. Kuhakikisha mikutano yote ikiwa ni pamoja na mikutano ya bodi, mafunzo, warsha na semina inafanyika katika kumbi za Serikali na Taasisi za Umma;

iv. Kutoa kipaumbele kwa Taasisi za Umma katika kununua huduma kama vile bima, usafirishaji wa barua, wavuti, simu, mizigo na vifurushi *(courier)*, matangazo na usafiri. Hata hivyo, ni muhimu kuzingatia unafuu na ubora wa gharama/huduma hizo;

v. Kuhakikisha Mashirika ya Umma yaliyoundwa kwa lengo la kujiendesha kibiashara, yanajiendesha kwa faida bila kutegemea ruzuku ya Serikali;

vi. Kudhibiti ununuzi wa bidhaa, huduma na ujenzi kwa lengo la kuhakikisha kuwa thamani halisi ya fedha ya ununuzi inapatikana kwa kutumia utaratibu wa *Force account*, ununuzi wa bidhaa wa pamoja/wingi, ushindani na kupitia masoko ya ndani;

vii. Kudhibiti matumizi ya umeme, simu na maji ikiwa ni pamoja na kutumia teknolojia inayopunguza matumizi ya nishati na kuhakikisha fedha zinazotengwa kwa ajili ya kulipia ankara hizo zinatumika kama ilivyokusudiwa;

viii. Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa mifumo ya umeme, maji na simu ili kuepuka matumizi yasiyo ya lazima;

ix. Kudhibiti ulipaji wa mishahara kwa kulipa watumishi wanaostahili;

x. Kununua nyumba kwa utaratibu wa kulipia kwa awamu (mortgage financing arrangement) hususan kwa majengo ya balozi na makazi ya wawakilishi walioko nje ya nchi badala ya utaratibu wa kupanga;

xi. Kudhibiti safari za nje ya nchi, ukubwa wa misafara na kuhakikisha kuwa safari hizo zinapata kibali kutoka Ikulu;

xii. Kuhakikisha ununuzi wa magari unafanyika kwa pamoja kupitia Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini *(GPSA)* baada ya kupata kibali cha ununuzi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu;

xiii. Kudhibiti utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu kwa kuhakikisha kuwa wanafunzi waliokidhi vigezo ndio wananufaika na mikopo hiyo; na

xiv. Kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika kufanikisha mawasiliano katika Ofisi za Serikali, hususan katika kipindi cha mpito cha Serikali kuhamishia shughuli za Makao Makuu Dodoma.

5.4 Kiwango cha Kubadilisha Fedha

38. Takwimu zote za kifedha sharti ziwasilishwe kwa kutumia sarafu ya shilingi ya Tanzania. Hivyo, maeneo ya bajeti yatakayolazimika kutumia fedha za kigeni yatumie kiwango cha kubadilisha fedha cha Shilingi za Tanzania 2,311.35 kwa Dola moja ya Kimarekani kwa mwaka 2017/18.

5.5 Kujumuisha Masuala Mtambuka Katika Mipango na Bajeti

39. Maafisa Masuuli wanapaswa kujumuisha masuala mtambuka katika mipango na bajeti ya mwaka 2017/18 na kuhakikisha utekelezaji wake unafanyika ipasavyo. Ili kufanikisha lengo hili, kila Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Umma zinasisitizwa kutenga fedha za kutekeleza vipaumbele kwenye masuala mtambuka. Vipaumbele hivyo ni pamoja na masuala ya kijinsia, watu wenye ulemavu, lishe, mazingira, mabadiliko ya tabia nchi pamoja na mapambano dhidi ya maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI. Aidha, Maafisa Masuuli waweke kipaumbele katika masuala yote yanayohusu watu wenye mahitaji maalum hususan ajira, afya, elimu, na ujenzi wa miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu.

5.6 Utawala Bora

40. Katika mwaka 2017/18, Serikali itaendelea kutekeleza maboresho ya masuala mtambuka ambayo ni ya muhimu katika utawala bora, uboreshaji wa huduma na uwajibikaji. Maboresho haya yanajumuisha: Programu ya Maboresho katika Utumishi wa Umma *(PSRP)*, Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa *(LGRP)*, Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria *(LSRP)*, Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP), Maboresho ya Sekta ya Fedha *(SGFRP)*, Uboreshaji wa Mazingira ya Biashara *(BEST)*, na Mkakati na Mpango Kazi wa Taifa wa Kupambana na Rushwa *(NACSAP)*.

41. Maboresho mengine ya kuzingatia ni pamoja na Udhibiti wa Fedha Haramu, Programu ya Uendeshaji wa Shughuli za Serikali kwa Uwazi *(OGP)*, Mfumo wa Nchi za Kiafrika wa Kujitathmini zenyewe

(APRM), na Mpango Kazi wa Taifa wa Haki za Binadamu. Hivyo, kila taasisi inapaswa kuzingatia majukumu yake na kuhakikisha inatenga fedha za kutekeleza kwa ukamilifu maboresho yanayowahusu.

5.7 Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

42. Serikali itaendelea kuwawezesha wananchi kiuchumi kupitia Mfuko wa Uwezeshaji Kiuchumi, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake, Mfuko wa Taifa wa Uwezeshaji Kiuchumi, Mfuko wa Kuwawezesha Kiuchumi Wajasiriamali Wadogo *(SELF)*, Mfuko wa Kusaidia Watu wenye Mahitaji Maalum, na Mfuko wa Rais wa Kujitegemea *(PTF)*.

43. Katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya Mwaka 2015, Serikali itaendelea kutenga Shilingi milioni 50 kwa kila kijiji, mtaa na shehia kupitia Mfuko wa Mzunguko *(Revolving Fund)*. Mfuko huo utasimamiwa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI na kutekelezwa katika ngazi za kijiji, mtaa na shehia. Maafisa Masuuli wanapaswa kuhakikisha kuwa fedha hizo zinawafikia walengwa na marejesho yanafanyika kwa wakati kulingana na miongozo na taratibu za Mfuko ili malengo yake yaweze kufikiwa na kuwezesha Mfuko kuwa endelevu. Aidha, Maafisa Masuuli wanapaswa kuzingatia kuwa miradi/biashara itakayofaidika inachaguliwa kwa kuzingatia vigezo na masharti ya Mfuko.

5.8 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

44. Tanzania ni mwanachama wa Umoja na Mataifa *(UN)*, Umoja wa Afrika *(AU)*, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika *(SADC)* na Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)*, hivyo imeridhia mikataba, itifaki na makubaliano mbalimbali baina ya nchi na nchi, Kikanda na Kimataifa. Mikataba ya Ushirikiano baina ya nchi na nchi imesainiwa katika kufanikisha maendeleo ya kiuchumi. Ili kuweza kushiriki ipasavyo katika makubaliano tajwa kipaumbele kitawekwa kwenye utekelezaji wa makubaliano ya Nchi na Nchi, Kikanda na Kimataifa ikiwemo Malengo ya Maendeleo Endelevu *(SDGs)* 2030, *AU Agenda* 2063, Dira ya *EAC* 2050, *"SADC- RISDP"*, *AGOA*, mikataba na itifaki zingine zilizoridhiwa.

45. Kwa kuzingatia makubaliano hayo, Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaagizwa kuzingatia yafuatayo:

i. Kuhakikisha bajeti zinatengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi yote ya makubaliano mbalimbali ya nchi na nchi, Kikanda na Kimataifa ikiwemo gharama za fidia kwa ajili ya Kituo cha Umoja wa Mataifa kinachotegemewa kujengwa Mjini Arusha katika eneo la Lakilaki;

ii. Kuhakikisha utekelezaji wa makubaliano mbalimbali yanayohitaji kuridhiwa yanawasilishwa Wizara inayo shughulikia mambo ya nje, Afrika Mashariki na ushirikiano wa kimataifa kwa hatua zaidi;

iii. Kuhakikisha ufuatiliaji wa jumla na uratibu katika utekelezaji wa makubaliano mbalimbali katika sekta zao yaliyosainiwa kati ya Tanzania na nchi nyingine pamoja na makubaliano ya Kikanda na Kimataifa;

iv. Kusimamia, kuratibu na kutathmini utekelezaji wa mikataba, itifaki na makubaliano yaliyopo chini ya sekta zao;

v. Kuhamasisha umma kwa kushirikiana na wadau wengine kuhusu fursa zilizopo katika nchi wanachama wa *EAC*, *SADC* na jumuiya za Kimataifa ambazo Tanzania ni mwanachama ili kunufaika nazo;

vi. Kutumia fursa za kifedha zilizopo katika ushirikiano wa Kimataifa, Kikanda na baina ya nchi na nchi;

vii. Kujenga uwezo wa maofisa waliopo katika balozi za Tanzania ili kuiwakilisha ipasavyo nchi katika mikutano na makongamano ya kimataifa;

viii. Kutenga bajeti ya mikutano na makongamano ya kimataifa ya msingi yaliyopo chini ya sekta zao; na

ix. Kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango miadi yote ya kuchangia michango ya Taasisi za Kimataifa na Kikanda kwa ajili ya kutengewa fedha na kulipwa.

5.9 Usimamizi wa Mali za Umma

46. Maafisa Masuuli wanapaswa kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya usimamizi wa mali za umma zilizo chini ya sekta zao. Aidha,

wanapaswa kupanga na kutenga fedha za kuhakiki, kupima, kuweka mipaka na kurasimisha umiliki wa mali za umma kwa ajili ya kuboresha usimamizi na utoaji taarifa. Mali hizo ni pamoja na viwanja vya Serikali; maeneo ya wazi, viwanda, shule, vyuo vikuu, hospitali, vituo vya afya, zahanati, jeshi na vyombo vya usalama; na mashamba ya umma. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI kupitia Halmashauri wanapaswa kuwezesha ukamilishwaji wa shughuli tajwa za Serikali.

47. Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa kushirikiana na Wizara mbalimbali inaelekezwa kuendelea kufanya ufuatiliaji wa wamiliki wa viwanda na mashamba yaliyobinafsishwa ili kuhakikisha yanafufuliwa na kufanya kazi. Aidha, Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji wanaelekezwa kuwasiliana na mifuko ya hifadhi ya jamii, taasisi za fedha na wadau mbalimbali ili kukubaliana maeneo wanayoweza kuwekeza kwa ajili ya kufufua viwanda na mashamba hayo.

5.10 Ushirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Binafsi

48. Maafisa Masuuli wanapaswa kutekeleza miradi iliyo katika utaratibu wa Ushirikiano baina ya Sekta ya Umma na Binafsi *(PPP)* iliyo chini ya sekta zao kwa kuzingatia Sheria ya *PPP* Na. 18 ya Mwaka 2010 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2014. Ili kukuza utekelezaji wa miradi ya *PPP*, vipaumbele vitatolewa kwa miradi ambayo inafanyiwa upembuzi yakinifu kama vile: mradi wa barabara ya tozo ya Dar es Salaam – Chalinze; mradi wa kiwanda cha kuzalisha dawa na vifaa tiba; Awamu ya Kwanza ya Mradi wa Mabasi yaendayo Haraka Dar es Salaam – Uendeshaji; na Mtambo wa Uzalishaji wa Umeme wa Gesi wa Kinyerezi III. Hivyo, kila Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Umma zinatakiwa kukamilisha upembuzi yakinifu ili kuwezesha miradi hiyo kutekelezwa kupitia mfumo wa *PPP*. Aidha, katika kuanzisha miradi ya *PPP* na kujenga uwezo wa kitaasisi, Serikali itaendelea kutenga fedha kwenye Mfuko wa Uwezeshaji wa *PPP*.

49. Kila Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazotarajia kushirikiana na sekta binafsi katika miradi zinapaswa kufanya maandalizi ya kutosha ikiwemo upembuzi yakinifu kabla ya kuingia makubaliano ya kutekeleza miradi hiyo. Maafisa Masuuli wanapaswa:

i. Kubainisha miradi itakayovutia uwekezaji wa sekta binafsi na kuiwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya uchambuzi kwa mujibu wa Sheria ya *PPP* Na. 18 ya Mwaka 2010 kama ilivyorekebishwa Mwaka 2014. Kwa upande wa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, miradi ya PPP inapaswa kuwasilishwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa ajili ya uchambuzi na uidhinishwaji kabla ya kuwasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango;

ii. Kujenga mazingira bora ya biashara ili kuvutia ushiriki wa sekta binafsi;

iii. Kujumuisha miradi ya *PPP* katika mipango na mikakati ya sekta zao; na

iv. Kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango gharama za upembuzi yakinifu, pengo la kugharamia mradi *(viability gap funding)*, madai ya huduma zilizotolewa *(availability payment)* na dhamana inayohitajika ya miradi ya PPP iliyo chini ya sekta zao.

5.11 Usimamizi wa Vihatarishi

50. Serikali ilitoa Mwongozo wa Uandaaji na Utekelezaji wa Usimamizi wa Vihatarishi *(Guidelines for Developing and Implementing Institutional Risk Management)* mwaka 2013 katika Taasisi za Umma kwa lengo la kuhakikisha kuwa suala la usimamizi wa vihatarishi linazingatiwa. Aidha, Mwongozo Na. 12 wa mwaka 2012/13 wa Mlipaji Mkuu wa Serikali ulibainisha majukumu ya Maafisa Masuuli na taratibu za utekelezaji. Hivyo, Maafisa Masuuli wanapaswa kuchukua hatua stahiki za kukabiliana na vihatarishi katika Mipango na Bajeti kwa mwaka 2017/18.

6.0 MAELEKEZO MAHSUSI KWA SEKRETARIETI ZA MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

51. Katika kipindi cha uandaaji wa Mipango na Bajeti kwa mwaka 2017/18, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zitatakiwa kuzingatia masuala yafuatayo:

i. Majukumu yao ya kimsingi ikiwa ni pamoja na kudumisha amani, utulivu na usalama katika maeneo yao ya utawala;

ii. Kuendesha mikutano ya kisheria ya Vijiji, Wilaya na Mikoa ili kuimarisha utawala bora na uwajibikaji katika ngazi zote;

iii. Kufanya mapitio ya Sheria ndogo za Mamlaka za Serikali za Mitaa ili ziendane na hali ya sasa hususan katika ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri katika maeneo yao;

iv. Kupitia na kuimarisha utekelezaji wa Sera ya Ugatuaji wa Madaraka kwa Wananchi *(D by D)* katika maeneo yao ya utawala kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma kwa kuzingatia kujenga uwezo katika ngazi za chini (vijiji na kata);

v. Kuandaa mipango kabambe ya maendeleo ya miji na kuijumuisha katika mipango mikakati kama njia ya kushughulikia maeneo yasiyopangwa mijini;

vi. Kuandaa Mipango Mikakati ya Mikoa na Serikali za Mitaa sambamba na Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2017/18, maelekezo ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya mwaka 2015;

vii. Kuimarisha maendeleo endelevu ya matumizi ya ardhi kulingana na mipango ya vijiji na miji, upimaji wa ardhi, na kutenga maeneo madogo, ya kati na makubwa kwa ajili ya viwanja na maendeleo ya kilimo na ujenzi wa miundombinu ya maji, shule, huduma za afya, vituo vya mabasi, masoko na sehemu za mapumziko sambamba na Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999;

viii. Kuanzisha na kurasimisha utengaji wa maeneo ya uwekezaji kwa ajili ya viwanda, kilimo, ufugaji, makazi, hifadhi ya wanyamapori na misitu, na vyanzo vya maji katika maeneo yote ya halmashauri ili kuzuia kutokea migogoro isiyo ya lazima na gharama za fidia;

ix. Kutekeleza mwongozo wa Serikali Mtandao katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma;

x. Kuboresha usafi wa mazingira kwa kuimarisha uwezo wa kitaasisi katika usimamizi wa taka – maeneo ya kukusanyia, kusomba na madampo ya taka, miundombinu ya taa za barabarani, vyoo vya jumuiya na mfumo wa maji taka;

xi. Kuimarisha timu za afya za Mikoa na Serikali za Mitaa ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya zilizoboreshwa katika Halmashauri, Mikoa na Hospitali za Rufaa pamoja na huduma maalum;

xii. Kuimarisha ubora wa afya na huduma za lishe na kuongeza upatikanaji wa huduma za lishe katika ngazi ya jamii na vituo vya kutolea huduma;

xiii. Kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na kuhakikisha kuwa asilimia 60 ya mapato inatengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo;

xiv. Kuendelea kukusanya kodi ya majengo kwa Halmashauri ambazo hazijafikiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Aidha, halmashauri hizo zinaelekezwa kutoa ushirikiano wa kuunganisha na kuhamisha mifumo ya kukusanya kodi ya majengo kwenda Mamlaka ya Mapato Tanzania;

xv. Kujenga, kurekebisha na kuimarisha miundombinu ya kijamii na kiuchumi hususan katika sekta ya elimu, maji, afya, kilimo, mifugo, uvuvi na barabara kwa kuzingatia ubora wa kitaifa;

xvi. Kuendelea na ujenzi, ukarabati na uwekaji wa vifaa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, Ofisi na Makazi ya Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Maafisa Tawala wa Mikoa na Wilaya; na Ofisi za Kata na Vijiji. Aidha, kipaumbele katika ujenzi kizingatie kukamilisha miradi ya maendeleo ambayo haijakamilika;

xvii. Kutekeleza shughuli ambazo fedha zake zilivuka mwaka kwa kuzingatia Kifungu cha 29(3) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 na Kanuni za Bajeti za mwaka 2015;

xviii. Kutenga fedha kwa ajili ya watu wenye ulemavu na mahitaji maalum ikiwemo vifaa vya mafunzo na mahitaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi;

xix. Kuanzisha na kuimarisha kamati za kijamii za usimamizi wa maji na kuhakikisha upatikanaji endelevu wa maji safi na salama;

xx. Kuimarisha usimamizi wa huduma za ugani zinazoendana na mahitaji ya soko na kuhakikisha zinaendana na Sera ya Ugatuaji wa Madaraka kwa Wananchi, pamoja na kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika kilimo na maendeleo ya viwanda;

xxi. Kuwekeza katika vyanzo vya mapato ili kuhakikisha upatikanaji endelevu wa mapato;

xxii. Kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya Mifuko ya Maendeleo ya Wanawake na Vijana;

xxiii. Kuthaminisha mali zote zinazohusiana na ardhi na kuhuisha kwenye daftari la kumbukumbu kwa ajili ya makusanyo ya kodi kwa Halmashauri zote za mijini na vijijini;

xxiv. Kuimarisha ukuzaji wa mazao ya kilimo na biashara na kuhakikisha usalama wa chakula;

xxv. Kukuza biashara ndogo na za kati, SACCOS, VICOBA na makundi mengine ya kijamii kwa ajili ya uzalishaji wa ajira;

xxvi. Takwimu kwa Sekta ya Elimu ziwe za hadi Januari 2017. Takwimu hizo ni pamoja na; idadi ya shule za Serikali, idadi ya wanafunzi wa shule za Serikali, idadi ya wanafunzi wa shule za bweni za Serikali, idadi ya Waratibu wa Elimu wa Kata;

xxvii. Uwasilishaji wa takwimu kwa Wizara ya Fedha na Mipango ufanywe kupitia Sekretarieti za Mikoa na kuidhinishwa na Ofisi ya Rais TAMISEMI; na

xxviii. Kuhakikisha kuwa fedha zinatengwa katika maeneo ya kipaumbele ili kuepuka uhamisho wa fedha wakati wa utekelezaji.

7.0 UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI TAARIFA YA UTEKELEZAJI

52. Ufuatiliaji na tathmini vitafanyika ili kuhakikisha kunakuwa na ufanisi wa utekelezaji kulingana na thamani halisi ya fedha za umma zinazotumika. Kwa msingi huu, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuhakikisha kuwa miradi ya maendeleo, programu na shughuli zote za Serikali zinabuniwa vizuri, kupangwa kwa mtiririko na kutenga fedha kwa kuzingatia bajeti iliyoidhinishwa.

53. Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Umma zizingatie Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mwongozo wa Uwekezaji wa Umma wa mwaka 2015 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ili kuwa na uwekezaji bora wa umma, utekelezaji thabiti na thamani ya fedha.

54. Maafisa Masuuli wanaagizwa kutenga fedha kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini na kuwatumia watumishi wenye ujuzi katika fani ya tathmini na ufuatiliaji. Aidha, wakati wa kutekeleza kazi hii wanatakiwa kuzingatia maelekezo kwa mujibu wa Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Miradi ya Umma wa mwaka 2015.

7.1 Utoaji wa Taarifa za Utekelezaji

55. Kwa mujibu wa Kifungu 55(4) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 na Kanuni ya 30(5) ya Sheria hiyo, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango taarifa za robo ya mwaka za utekelezaji wa bajeti ndani ya siku 30 kila baada ya robo ya mwaka. Aidha, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango taarifa ya utekelezaji ya mwaka katika kipindi kisichozidi tarehe 15 Oktoba baada ya kumalizika kwa mwaka wa fedha.

56. Taarifa za utekelezaji za robo mwaka na mwaka mzima zitawasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango; Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Ofisi ya Rais – TAMISEMI (kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa); na Ofisi ya Msajili wa Hazina (kwa Taasisi za Umma) zikiwa katika nakala ngumu na laini. Maafisa Masuuli wote wanatakiwa kuwasilisha taarifa hizo kwa mujibu wa muundo uliooneshwa katika kiambatisho cha mwongozo huu.

8.0 HITIMISHO

57. Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Umma zinaelekezwa kuzingatia Mwongozo huu pamoja na kiambatisho chake. Vile vile, zinaelekezwa kuimarisha utekelezaji wa mipango yao kwa kujielekeza katika maeneo ya kimkakati na miradi ya kielelezo iliyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na mikakati mingine inayolenga kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025.

58. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuhakikisha kuwa miradi ya maendeleo inaandaliwa na kuidhinishwa kikamilifu, na rasilimali fedha zilizotengwa katika mafungu yao zinatumika kwa uangalifu mkubwa na ufanisi.